

# Maelezo katika Swahili

Tume la uchaguzi la Queensland (Electoral Commission of Queensland ECQ) hufanya uchaguzi wa jimbo, uchaguzi wa serikali za mitaa pamoja na uchaguzi wa viwanda katika Queensland.

Uchaguzi wa serikali za mitaa unaofuata utafanyika tarehe 28 Machi 2020.

Uchaguzi wa jimbo unaofuata utafanyika tarehe 31 Oktoba 2020.

## Je, lazima nijiandikishe?

Ni lazima kujiandikisha pamoja na kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa, jimbo pamoja na uchaguzi wa shirikisho ikiwa wewe:

- ni raia wa Australia au mtendaji anayestahili kutoka Uingereza
- una umri wa miaka 18 au zaidi, pamoja na
- umeishi katika anwani yako kwa angalau mwezi mmoja.

Zaidi ya hayo, watu wenye umri wa miaka 16 na 17 wanaweza kujiandikisha kwa kuandaa pamoja na kupokea haki kamili ya kupiga kura katika sikukuu ya kuzaliwa yao ya 18.

## Jinsi ya kujiandikisha

Wewe unaweza kujiandikisha kupiga kura kwa kujaza fomu ya uandikishaji kwa Kiingereza ([enrolment form in English](#)) au mtandaoni kwenye tovuti ([website](#)) ya Tume la uchaguzi wa Australia.

## Je, nitafanya kupiga kura vipi?

Kuna njia nyingi za kupiga kura, hata kama uko ng'ambo siku ya uchaguzi. Hii ni pamoja na upigaji kura wa mapema (kabla ya uchaguzi), kupiga kura katika kibanda cha kupigia kura siku ya uchaguzi, upigaji kura wa posta au kupiga kura kwa kupiga simu kwa wapiga kura stahifu.

Habari zaidi kuhusu upigaji kura katika Queensland inapatikana katika ECQ Mwongozo wa Upigaji Kura wa Lugha Nyingi ([Multilingual Voting Guide](#)).

## Je, unahitaji mkalimani?

Ikiwa wewe unataka habari zaidi, unaweza kuwasiliana na ECQ kupitia mkalimani, kwenye simu 0730821426.

## Wasiliana na sisi

ECQ iko katika Level 20, 1 Eagle Street, Brisbane QLD 4000.

Wewe unaweza kupigia simu ECQ kwenye 1300 881 665, kutuma baruapepe kwa [ecq@ecq.qld.gov.au](mailto:ecq@ecq.qld.gov.au) au ututumie faksi kwenye (07) 3036 5776.

Ikiwa wewe upo nchi ya ng'ambo, tupigie simu kwenye +617 3035 8103.